Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 5, Issue 2

4th Muharram 1432

10th December, 2010

Shariya ya ki-Islamu juu ya 'AQEEQAH

Sheikh Muhammad al-Jibaaly

KUMSHUKURU ALLAAH (سبحانه وتعالى)

Kumshukuru Allaah (سبحانه وتعالى) ndio shabaha kubwa ya ibaadah. Shukrani hudhihirisha kuwa mtiifu na kuwa mnyenyekevu juu ya fadhila za Allaah (سبحانه وتعالى), kuwa maridhia na kuwa na mahaba.

Inatupasa kujitahidi ilituwe na shukrani katika hali na kadhia zote za kimaisha. Shukrani hutolewa kwa ndimi kwa kutumia maneno ya sifa, mazinduo, na kutukuza. Pia hutolewa kwa kutumia miili na viungo kwa njia ya vitendo vyenye kuonyesha unyenyekevu, na utiifu kwa Mola (سبحانه وتعالى).

SIFA WALIZOKUWANAZO MITUME NA WAUMINI.

Shukrani ni sifa ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) aliyoisifu, na kwa sifa hiyo Akawaitisha Mitume wake na wafuasi wao. Kwa mfano, Alimsifu kipenzi chake *Khaleel*, Ibraahim (عليه السلام): **"(Alikuwa) mwenye kuzishukuru neema Zake (Allaah), akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyoka."**[1]

Na Akamsifu Mtume wake Nuh (عليه السلام): **"Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani."**[2]

Allaah (سبحانه وتعالى) aliwaamrisha waumini, kama alivyowaamrisha Mitume, wajipambe na wema wa shukrani: **"Enyi mlioamini! kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Allaah."**[3]

"Basi nikumbukeni (kwa kunishukuru kwa hii neema nilivyokuneemesheni ya kukuleteeni Mtume) (Nami) nitakukumbukeni; na nishukuruni wala msinikufuru."[4]

BAINA YA SHUKRANI NA KUTOSHUKURU

Allaah (سبحانه وتعالى) ameahidi kuongeza fadhila Zake kwa ajili ya kumshukuru Yeye: **"Kama mkishukuru, nitakuzidishieni."**[5]

Na Akawalaumu na kuwasuta wale wenye utovu wa shukrani: **"Kisha Akamtengeneza na Akampulizia roho Yake, na Akakupeni masikio na macho na nyoyo; ni kidogo tu shukrani zenu (kwake Yeye)."**[6]

WATOTO NI BARAKA KUTOKA KWA ALLAAH

Miongoni mwa neema kubwa kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) ni kizazi chema: **"Mcheni Yule ambaye amekupeni haya mnayoyajua. Amekupeni (chungu ya) wanyama na watoto wanaume."**[7] **Na Allaah Amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na Akakujaalieni kutoka kwa wake zenu watoto na wajukuu."**[8]

MALEZI YA WATOTO KWA NJIA YA SHUKRANI

Mu'min hujitahidi kuwa na malezi mema juu ya kizazi chake, na kuwafanya wawe ni watoto watiifu, wawe ni wenye kudumisha swala zao, na kuwa walinzi wenye majukumu ya *Da'wah* ya Uislamu. Huwalea watoto juu ya uongofu huu wa kutoka kwa Allaah haliyakuwa na Shukrani: **"Na (wakumbushe), Luqmani alipomwambia Mwanawe; na hali ya kuwa anampa nasiha. Ewe mwanangu! Usimshirikishe Allaah, maana shirki ndiyo dhuluma kubwa... Ewe mwanangu! Simamisha swala, na uamrishe mema, na ukataze mabaya, na usubiri juu ya yale yatakayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika tu taabu); Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu)."**[9]

Yaliyomo

Shariya ya Ki-Islamu juu ya 'Aqeeqah 1 – 4

Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Waamrisheni watoto wenu waanze kuswali watakapotimia umri wa kiaka saba; na wapigeni (iwapo hawatoswali) watakapotimia umri wa miaka kumi.[*10] Miongoni mwa jinsi ya kutoa shukrani kwa Allaah (سبحانه وتعالى) baada ya kubarikiwa watoto ni kwamba wazazi huchinja wanyama kwa niaba yao pindi wanapozaliwa. Hii ndiyo inayoitwa katika *Shariya ya ki-islamu* - ***'Aqeeqah***. Ni Sunnah ambayo iliyosahauliwa miongoni mwa waislamu wengi.

MAANA YA 'AQEEQAH

Mzizi wa neno 'aqeeqah katika lugha ya Kiarabu umetokamana na kitendo 'aqqa, (kitendo) kilicho na maana ya kutengana au kukata. Kulingana na al-Asmaa'ee, az-Zamakhsharee, na wengineo, limetokana na neno kama hilo linalozisimulia nywele za mtoto mchanga pindi anapozaliwa. Rai hiyo ya kwanza ndiyo yenye nguvu zaidi, kama ilivyoashiriwa na Ahmad, Ibn 'Abd il-Barr, al-Khattaabee, na wengineo [11]. Katika lafdhi ya Ki-Islamu, makusudio ya 'aqeeqah ni yule mnyama aliyechinjwa kama sadaka ya mtoto aliezaliwa. Imepewa jina hilo kwa sababu shingo yake (yule mnyama) ilikatwa wakati wa kuchinja. Vilevile inaitwa *naseekah* (uchinjaji).

HUKMU YA 'AQEEQAH:

Wanavyuoni wamekhitalifiana iwapo 'aqeeqah ni Sunnah (nafl) au ni Waajib.

Ushahidi yakwamba ni Waajib.

Wale walioshikilia yakwamba 'aqeeqah ni waajib, wamezitegemeza rai zao juu ya Ahaadeeth zifuatazo:

1. Imepokewa na Salmaan bin 'Aamir Ad-Dabbee yakwamba Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"'Aqeeqah inampasa kila mtoto. Kwahivyo mwaga*

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

damu kwa niaba yake; na umuondolee kitu [12] *chenye kumletea madhara."* [13]

2. 'Aaisha, Umm Karz, Asmaa' Bint Yazeed, na Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهمaa), wote wamepokea kutoka kwa Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"('Aqeeqah ni) kondoo wawili (waliolingana* [14]*) kwa mtoto wa kiume, na mmoja kwa mtoto wa kike. (Hapana neno iwapo wanyama hao watakuwa ni wake au waume)."* [15]

3. Samurah bin Jundub (Radhiallaahu 'anhu) amepokea yakwamba Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kila mtoto huwa amewekwa rehani kwa 'aqeeqah yake. Anapasa kuchinjiwa ifikapo siku yake ya saba, anyolewe nywele, na apewe jina (siku hiyo ya saba)*. [16]

'Abbaas, 'Aaisha, Anas, 'Alee, na wengineo (رضي الله عنهم), wamepokea yakwamba: "Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) alifanya 'aqeeqah ya al-Hasan na al-Husayn (kondoo wawili, kondoo wawili) [17]
Kutokana na riwaya hizi, ni wazi yakwamba Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) aliwaamrisha watu watekeleze 'aqeeqah, akaashiria yakwamba ni waajib kwa mtoto aliyezaliwa, na yeye mwenyewe akalitekeleza jambo hilo kwa wajukuu zake al-Hasan na al-Husayn.
Ni jambo lililothubutu katika *fiqh ya Ki-Islamu* yakwamba maamrisho kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) ni madokezo yakwamba hayo ni maamrisho yaliyo waajib - maadamu hakuna ushahidi wa ziada wenye kuiteremsha daraja kutoka katika hali ya kuwa waajib na kuwa jambo la khiyari. Kuhusu suala la 'aqeeqah, ushahidi uliotangulia umeliweka (suala hilo) kama jambo la waajib. Na kwa yafuatayo, tutajadiliana kuhusu ushahidi wenyewe.

Ushahidi yakwamba ni jambo la Khiyari.

Amma kwa Wanavyuoni walio na msimamo yakwamba 'aqeeqah ni jambo la khiyari, wanaamini yakuwa riwaya zifuatazo zimeiteremsha kutoka katika daraja ya wujoob (waajib) hadi kwenye daraja ya kuwa jambo lenye kupendekezwa:

1. Akapokea 'Amr Bin Shu'ayb kutoka kwa babake, kutoka kwa babu yake, aliesema yakwamba Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) aliulizwa kuhusu 'aqeeqah. Nae (صلى الله عليه وسلم) akajibu kwa kusema: *"Allaah Hapendi 'Uqooq* [18]*; yeyote aliyeruzukiwa mtoto, na akapendelea kumchinjia, basi na afanye hivyo - kondoo wawili waliolingana kwa mwanamume, na kondoo mmoja kwa mwanamke."* [19]

Akapokea Abu Raafi' (رضي الله عنه): "Wakati Faatimah (رضي الله عنها) alipomzaa al-Hasan (رضي الله عنه), alimuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) , 'Sifai mimi kummwagia mwanangu damu (kama 'aqeeqah)?' Akamjibu: "*La! Mnyoe nywele zake za kichwani tu, na utoe sadaqa inayolingana na uzani wake wa fedha*". Faatimah akafanya hivyo; na alipozaliwa al-Husayn, akafanya tena hivyo hivyo." [20]

Wale wanavyuoni walioshikilia yakwamba 'aqeeqah ni jambo la khiyari, wanabishana yakuwa katika hadeeth ya kwanza, maneno yenye nguvu, yamelifanya jambo hilo kuwa ni la khiyari na kutegemea matakwa ya mtu. Hatahivyo, maoni hayo hayawezi kukabiliana na ushahidi uliopita, kwa sababu itafahamika kumaanisha yakwamba, "Yeyote apendeleae kuchinja kwa sababu ana uwezo." Vilevile mabishano yao mengine ni kwamba, katika riwaya ya pili, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimzuiya mwanae asifanye 'aqeeqah. Hatahivyo, riwaya ya hapo awali ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) na Maswahaba wengine, akiwemo mumewe 'Alee (رضي الله عنه), inaonyesha waziwazi yakwamba sababu iliyomfanya kumzuiya ni vile ambavyo alikuwa tayari ashamfanyia yeye mwenyewe 'aqeeqah.

UAMUZI WA MWISHO:

Kama mulivyoletewa hapo juu, ushahidi unaonyesha waziwazi yakwamba 'Aqeeqah ni waajib; na ule ushahidi uelezao vyengine haukuwa na nguvu za kuweza kupunguza daraja yake na kulifanya jambo hilo kuwa ni la khiyari. Kwahivyo, kwa yeyote awezae kufanya 'Aqeeqah kwa watoto wake, basi na afanye hivyo; Na Allaah (سبحانه وتعالى) yote yamueleya.

Ama kwa yule asiyekuwa na uwezo, basi huyo amesamehewa (amepewa ruhusa); lakini akitaka anaweza kukopa pesa ili alitekeleze jambo hilo. Imaam Ahmad (رحمه الله) aliulizwa kuhusu mtu aliyekopa pesa ili kuitekeleza 'aqeeqah nae akajibu: "Natumai yakwamba Allaah (سبحانه وتعالى) atamstawisha (Atampa uwezo), kwa ajili ya kuihuisha Sunnah."

Aina ya wanyama wanaotolewa kwa 'Aqeeqah

AINA: Wanyama waliotajwa kwa ajili ya 'aqeeqah katika Sunnah ni ***Kabsh*** (kondoo dume) na ***Shah au (Shaat)***. Kulingana na Ibn Manzoor katika Lisaan ul-'Arab: "Maana ya Shah ni kondoo mmoja; na anaweza kuwa ni jike au dume...; Na inasemekana yakwamba Shah huwenda akawa ni katika kondoo, mbuzi, kulungu (mnyama mfano wa paa), Ng'ombe, wanyama wa kilimo, au pundamilia."

Kitendo cha kawaida miongoni mwa ma-Salaf kwenye 'aqeeqah zao ni kuchinja kondoo na mbuzi. Lakini nakala za hadeeth hazikutenga uchinjaji wa wanyama walio wakubwa.
IDADI: Kama ilivyonukuliwa katika riwaya zilizotufikia hapo awali kutoka katika matamshi na vitendo vya Mtume (صلى الله عليه وسلم), yakwamba 'aqeeqah ya mtoto wa kiume ni wanyama wawili na mtoto wa kike ni mnyama mmoja. Tafauti iliyoko baina ya wake na waume katika 'aqeeqah na ilinganishwe na tafauti baina yao kwenye mas-ala ya utoaji ushahidi, urathi, fidia (ya damu), n.k (na Kadhaalika). Mambo hayo huja yakajitokeza kwenye haki za kijamii na madaraka, na wala hapana dhamana yoyote ya kuthamini kitu au malipo zaidi kuliko kingine - kilicho bora na ambacho ni chenye kutegemewa ni wema wa mtu.

HALI YA KUWA KIUME AU KIKE

Kama ilivyokwisha kuashiriwa hapo awali kwenye hadeeth ya 'Aaisha, Umm Karz, na wengineo, **"Hapana madhara iwapo ni wanyama waume au wake."**

UMRI, UKUBWA, nk.

Hapana riwaya iliyo saheeh kuonyesha sifa nyengine za 'aqeeqah, kama vile

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

ukubwa, umri, rangi, nk. Rai ya baadhi ya wanavyuoni ni kwamba yahitajika kuwa na sifa kama zile za *udhiyah* [21]. Hoja hiyo haina ushahidi wowote, na vitendo vya ibaadah visivyokuwa na ushahidi havifai kufungamanishwa na *Qiyaas* (kukisia ki-akili). Walaakin, ni muhimu yakwamba 'aqeeqah yenyewe, kwa vile ni kichinjo kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyo *udhiyah* , inampasa mwenye kuchinja atafute mnyama mwenye sifa bora kulingana na uwezo wake.

Ni lini 'Aqeeqah inapostahiki kutekelezwa

Katika hadeeth ya Samurah iliyotajwa hapo awali, Rasoolullaahi (صلى الله عليه وسلم) ameamrisha 'aqeeqah itekelezwe *"... Katika siku ya saba ..."* baada ya mtoto kuzaliwa. Akasema Waliyy Ullaah id-Dahlawee (رحمه الله): "Hilo ni jambo linalotekelezwa siku ya saba ili kuipa jamii wakati wa kutosha kurudisha afya njema baada ya machofu ya mazazi, na kuwapa wasaa wa kutafuta wanyama wanaohitajika kwa 'aqeeqah."

Zaidi ya hayo, akapokea Buraidah (رضي الله عنه) yakwamba Rasoolullaahi (صلى الله عليه وسلم), amesema:

"'Aqeeqah na ifanywe siku ya saba, au ya kumi na nne, au ya ishirini na moja (baada ya mazazi)"[22]

Iwapo mtu ataziacha kwa kusudia nafasi hizo tatu, basi haitomlazimu kufanya 'aqeeqah tena siku nyengine. Hatahivyo, kama mtu hakuweza kupata wanyama, au alisahau, au alikosea kuhisabu masiku, au hakujua yakwamba aliwajibika, mtu huyo anaweza kuitekeleza 'aqeeqah pindi atakapokumbuka au atakapokuwa na uwezo, kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) haikalifishi nafsi kupita kadiri ya uwezo wake.

Ni muhimu kwa watu kufahamu yakwamba nyakati hizi zilipangwa makhsusi kwa uchinjaji wa wanyama. Ama kuhusu mapishi (kupika) na makulati (kula), hayo hayakupangiwa nyakati, na yanaweza kufanywa wakati wowote mwengine baada ya kuchinja.

YAPASAYO KUFANYWA KATIKA 'AQEEQAH

UGAWANYAJI WA NYAMA

Kwa ulinganishaji na sifa kama zile za *udhiyah*, baadhi ya wanavyuoni wamependekeza kuigawa 'aqeeqah kwa mafungu matatu: fungu moja wakala wenyewe, fungu jengine wakalisha watu, na kujitolea sadaka fungu jengine. Hilo ni jambo lisilo na ushahidi wowote, isipokuwa kwa hadeeth moja iliyo dhaif iliyopokewa na al-Haakim kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها).

Kwahivyo, inaruhusiwa kwa mwenye kufanya 'aqeeqah kuigawanya kulingana na uwezo wake wa kifedha, wakati, nk. Anaweza kujiekea yote, kujitolea yote, kuwapikia na kuwalisha watu, nk (na kadhaalika).

KUWALISHA WATU

Wanavyuoni wengi wamependekeza kuwalisha watu katika 'aqeeqah. Hata kama hakuna maandishi makhsusi katika Sunnah yanayoamuru jambo hilo, kuna maandishi yanayowahimiza, ki-ujumla, Waislamu kuwalisha watu. Ibn ul-Qayyim (رحمه الله) amesema: "Imependekezwa kuipika nyama badala ya kuwapa watu nyama mbichi, hapo itakuwa masikini na majirani wamepunguziwa shughuli za mapishi: Hichi ni kitendo cha kuzidisha wema na shukrani kwa baraka, na alama ya tabia njema na ukarimu. "

Lakini hatahivyo, fikra za ki-makosa za baadhi ya watu yakwamba malengo ya 'aqeeqah ni kuwaandalia watu karamu au mfano wa *waleemah* . Hujishughulisha zaidi na hayo kuliko uchinjaji wenyewe, wengine hununua nyama badala ya kuchinja. Hayo ni makosa, kwani huko ni kukhalifu msingi uliowekwa wa 'aqeeqah: Kuchinja.

KUPAKA DAMU KICHWANI?

Kitendo cha zama za kabla ya Uislamu ilikuwa ni kukipaka kichwa cha mtoto mchanga damu ya 'aqeeqah. Uislamu ukaharamisha kitendo hicho, kama ilivyopokelewa na Buraydah (رضي الله عنه):

"Katika zama za Jaahiliyyah, moja wetu anapopata mtoto, huchinja kondoo kisha akampaka damu (ya kondoo) kichwa chake (yule mtoto). Ulipokuja Uislamu, tuliamrishwa kuchinja kondoo, kumnyoa mtoto kichwa chake, na kukienezea za'farani (saffron)." [23]

Vilevile, Yazeed Bin 'Abdillaah al-Muzanee alihadithia yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mtoto na afanyiwe 'aqeeqah; lakini kichwa chake na kisiguswe na damu"* [24]

HIKMA YA KUFANYA 'AQEEQAH

Wanavyuoni wametoa maoni yao ya ki-hikma kuhusu kanuni za *'aqeeqah* katika Uislamu. Kwa yafuatayo, tunawaletea yaliyo muhimu zaidi katika yale yaliyopendekezwa na Ibn ul-Qayyim na Waliyy Ullaah id-Dahlawee:

1. Ni njia ya busara ya kuidhinisha mazazi na nasaba ya mtoto mchanga. Bila ya shaka hiyo ni njia bora kuliko kufanya matangazo kwenye soko (au kufanya matangazo kwenye vyombo vya habari, magazeti, nk).

2. Huongeza ukarimu na kukomesha ubakhili.

3. Ni kitendo chenye kumpambanua Muislamu kutokamana na Kafiri katika nyakati za Jaahiliyyah, ambao walikuwa wakimpaka mtoto damu (ya mnyama) kichwani, au Manasara (Makristo) ambao hubatiza watoto wao na maji.

4. Ni kitendo cha sadaka kinachowakumbusha wazazi kuhusu sadaka ya Mtume Ibraahim (عليه السلام) - Na huko ni kuimarisha uhusiano na walio wema, na kuendelea kuwahimiza kutenda mema.

5. Ni sadaka inayosaidia kumlinda mtoto - kama vitendo vyengine vya utiifu na wema.

Ni fidia kwa mtoto na humkomboa kutoka kwenye amana, ili awe na wadhifa wa kuweza kuwaombea wazazi wake siku ya Qiyaamah. Akasema Imaam Ahmad (رحمه الله): "Maana ya 'Amana' kwenye hadeeth [25] ni kwamba mtoto huwa katika kizuizi cha kutoweza kuwaombea wazazi wake."

Na akasema Ibn ul-Qayyim: "Maana iliyo wazi kutoka kwenye hadeeth hiyo ni kwamba mtoto mwenyewe huwa katika vizuizi vya mambo mema amabyo pengine angeliyapata yeye. Wala haimaanishi yakuwa yeye ataadhibiwa siku ya kiyama."

Baadhi ya Sunnah za mtoto mchanga

Mbali na kufanya 'aqeeqah, kuna mambo mengine yaliyosisitizwa katika Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusiana na mtoto mchanga aliyezaliwa. Kwa mfano, wamehadithia

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Anas na Sahl (رضي الله عنهم):
Baadhi ya watoto wachanga waliozaliwa waliletwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم); nae akawapa majina na akala tende (akazitafuna) na kuwapangusa nazo (mate ya tende) midomoni mwao. [26]

KUWAPA MAJINA MAZURI: Imehimizwa katika Sunnah kuwachagulia watoto wachanga majina mazuri.
Baadhi ya majina yaliyopendekezwa ya watoto wa kiume ni 'Abdullaah, 'Abd ur-Rahmaan, Haarith, Hammaam, majina ya Mitume na majina ya Maswahaba.
Baadhi ya majina yaliyopendekezwa ya watoto wa kike ni Maryam, Saarah, majina ya mabinti wa Mitume na Wake zao (رضي الله عنهم), na majina ya Wanawake wa Maswahaba.

KUNYOA KICHWA: Imependekezwa kunyoa vichwa vya watoto wachanga, iwapo ni mke au mume, katika siku ya saba, na kuwatolea *sadaqah* kiasi cha uzani wa nywele unaolingana na fedha. Imeshatajwa hapo awali katika amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa binti yake Faatimah (Radhiallaahu 'anha).

SUNNAH NYENGINE: Vilevile imependekezwa kuwapasha tohara watoto wa kiume katika siku ya saba, na kuwafanyia *tahnik* (kuwarambisha kitu kitamu kwenye mdomo).
Ama kuhusu kuadhini katika sikio la mtoto mchanga la upande wa kulia na kufanya *iqaamah* kwenye sikio la kushoto, riwaya zilizopokewa kuhusiana na suala hilo ni dhaifu, haswa hiyo riwaya kuhusu *iqaamah*

NUKTA MUHIMU

1. An-Nahl 16:121
2. Al-Israa 17:3
3. Al-Baqarah 2:172
4. Al-Baqarah 2:152
5. Ibraahim 14:7
6. As-Sajdah 32:9
7. Ash-Shu'araa' 26:132-133
8. An-Nahl 16:72
9. Luqmaan 31:13-17
10. Imepokewa na Abu Dawud; Saheeh
11. Tizama Fat-h ul-Baaree 9:501
12. Yaani, mnyoe nywele zake
13. Imepokewa na at-Tirmidhee na an-Nasaai (Saheeh ul-Jaami' no.4253)
14. Yaani wanaolingana kwa ukubwa na maumbile
15. Imepokewa na Ahmad, na Abu Dawud, an-Nasaai, at-Tirmidhi, na wengineo (Saheeh ul-Jaami' no.4105-4107, na Irwa ul-Ghaleel no.1166)
16. Imepokewa na an-Nasaai, Abu Dawud, Ibn Maajah, na wengineo (Saheeh ul-Jaami' no.4541, na Irwa ul-Ghaleel no.1165)
17. Imepokewa na an-Nasaai, Abu Dawud, na wengineo (Irwa ul-Ghaleel no.1164). Angalia jinsi riwaya nyengine zimetaja "Kondoo mmoja, kondoo mmoja." Lakini kilicho hapa ndicho kilichosibu zaidi, kulingana na maoni ya Ibn ul-Qayyim, al-Albaanee nk.
18. Vitendo viovu, haswa kuwatendea wazazi. Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) alilifahamu vyema suali hilo; lakini alichukua nafasi hiyo kutaja makatazo ya madhambi hayo yanayotokamana na mzizi huohuo wa neno lenye maana ya **'aqeeqah**
19. Imepokewa na Ahmad, an-Nasaai, Maalik, na wengineo. Imesahihishwa na al-Albaanee katika as-Saheeha no.1655
20. Imepokewa na Ahmad na wengineo. Ikapewa hukmu ya Hassan (nzuri) na al-Albaanee katika Irwaa ul-Ghaleel no.1175
21. Uchinjaji unaotekelezwa katika siku ya Adhaa (siku kuu)
22. Imepokewa na at-Tabaraanee na wengineo. Ikahukumiwa kuwa Saheeh na al-Albaanee (Saheeh ul-Jaami' no.4132)
23. Imepokewa Abu Dawud, al-Haakim, na wengineo. Ikasahihishwa na al-Albaanee katika (Saheeh ul-Jaami' no.1165)

KILIFI BOOKS & STATIONERY STORE LTD

Executive Director: Muhammad A. Said

Suppliers of: *School Textbooks & Stationeries, Office Stationeries, Films, Dealers of AirTel Cards and Safaricom Cards.*

* Madrasatul Munawwar Wakf Building—Mombasa

* Jamo Kenyatta Avenue—Mombasa

* Hospital Street—Opposite P.H.D Mombasa.

P.O.Box 99900 *Tel: 041-2495763*

Postal Code: 80107 *Fax: 041-2495764*

E-mail:kilifibks@africaonline.co.ke *Mobile: 0722-265103 / 0722-669414*